# Jarida Maalum

## SHIRIKA LA POSTA TANZANIA

www.posta.co.tz Toleo la 0005 | Oktoba - Desemba 2022



Posta Kiganjani, Twenzetu Kidigitali

# TIMU YA WAHARIRI

**MWENYEKITI**
Macrice D. Mbodo
Postamasta Mkuu, Shirika la Posta Tanzania

**MRATIBU NA MHARIRI WA JARIDA**
Elia P.K. Madulesi
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano,
Shirika la Posta Tanzania.

**MSANIFU WA JARIDA**
Loema Joseph

**WAHARIRI**
Mashala Lufunga, Jane Sallu,
Rachel Kitinya & Khadija M. Suedi

Posta Let's Go!

# WAZIRI NAPE: POSTA KIGANJANI KUNUFAISHA ZAIDI YA WATU MILIONI 37 NCHINI




Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye ametoa takwimu ya watumiaji wa simu janja ambao hutumia simu hizo kwa lengo la manunuzi pamoja na kupata huduma mtandao ndani na nje ya nchi.

Ameyasema hayo tarehe 09 Oktoba, 2022 alipokuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya Siku ya Posta Duniani ambayo yaliambatana na Uzinduzi rasmi wa Huduma ya Posta Kiganjani pamoja na uzinduzi wa Stempu ya Pamoja baina ya Tanzania na nchi ya Oman na Stempu ya vivutio vya Utalii katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Posta Kiganjani ni muundombinu "APPLICATION" unaowezesha inawezesha kupata huduma zote katika kifaa chochote cha TEHAMA ambapo huduma hiyo inapatikana kwa kupakua "APP" ya Smart Posta katika "Play Store" au "App Store".

Akizungumza wakati wa maadhimisho hayo Mhe. Nape ameeleza kuwa, wananchi wengi wana simu janja ambazo ndiyo msingi wa upatikanaji wa huduma mtandao, hivyo huduma ya Posta Kiganjani itarahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi ambapo zaidi ya watanzania milioni 58 wanamiliki simu janja huku wananchi milioni 37 wakitumia simu hizo kupata huduma za mtandao pekee.

Aidha, Mhe. Waziri Nape, amelitaka Shirika la Posta Tanzania kubuni biashara na huduma mpya zenye kuendana na maendeleo ya teknolojia ili kuendana na vionjo vya wateja katika kukidhi mahitaji yao kwa wakati na ubora zaidi.

Vilevile, Mhe Nape amemshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan  Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania, kwa kuongoza zoezi la uwekaji wa mfumo wa Anwani za Makazi ambalo limekuwa muundombinu muhimu katika huduma za Posta nchini ikiwemo Biashara Mtandaoni.

Katika hatua nyingine Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ametumia nafasi hiyo kulipongeza Shirika la Posta nchini kwa jitihada zake za kukuza na kutunza uhusiano wa kihistoria uliopo baina ya Tanzania na nchi ya Oman kwa kuandaa Stempu maalum ya Pamoja yenye kumbukumbu la Jengo la Maajabu (House of Wonders) lililopo mjini Zanzibar.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Moshi Kakoso amelitaka Shirika la Posta Tanzania kuendelea kuwa na ubunifu na jitihada katika utendaji wake pamoja na kutumia fursa zilizopo katika kulikuza Shirika kiuchumi, huku akiahidi kuendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa faida ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Naye, Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Jim Yonazi amesema kuwa, katika kuendeleza mpango wa Uchumi wa kidijitali nchini inatarajiwa kuwa uchumi huo utachangiwa kwa sehemu kubwa na sekta ya Posta nchini na tayari kuna mipango thabiti ya kuhakikisha sekta ya Posta inaendelea kukua.

Kwa upande wake, Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Ndg. Macrice Mbodo ameeleza namna ambavyo Shirika hilo linavyoendelea kuboresha huduma zake sambamba na maendeleo ya Teknolojia ili kuwapunguzua usumbufu wananchi katika kupata huduma pale wanapohitaji, huduma hizo ni pamoja na Duka Mtandao linalowapa fursa wananchi kuuza na kununua bidhaa mtandaoni, kuboresha mifumo ya kiusalama, kuanzisha kituo cha Huduma Pamoja kinachowapa fursa wananchi kupata huduma zote za Serikali mahali pamoja na sasa Shirika limezindua rasmi huduma ya Posta Kiganjani. ukiwa ni mwendelezo wa kuleta huduma za Kidijitali karibu na wananchi.

# MATUKIO KATIKA PICHA WAKATI WA MAADHIMISHO YA SIKU YA POSTA DUNIANI

Naye Naibu Balozi wa Oman nchini Tanzania Ndg. Rashid Al- Manji ameishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuendelea kuiwezesha sekta ya Posta katika utoaji wa huduma zake. Pia ameahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kuhakikisha sekta ya Posta inakua katika nchi hizi mbili.




Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye akizungumza wakati wa Maadhimisho hayo.




Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Jim Yonazi akizungumza wakati wa Maadhimisho hayo.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye akipokea maelezo ya huduma ya Posta kiganjani kutoka kwa Meneja Huduma za Barua na Usafirishaji Bw. Jasson Kalile wakati wa Maadhimisho hayo.



Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Mbodo akizungumza wakati wa Maadhimisho hayo.

# MHANDISI KUNDO: BORESHENI HUDUMA ZA POSTA ILI ZIANDANE NA MABADILIKO YA TEKNOLOJIA YALIYOKO DUNIANI KWA SASA






Naibu Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Mhandisi Kundo Andrea Mathew ameyataka Mashirika ya Posta ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuchangamkia fursa za mabadiliko ya teknolojia yanayoendelea duniani kwa sasa ili sekta hiyo iweze kutoa huduma bora zinazokidhi matakwa ya wateja.

Mhandisi kundo ameyasema hayo tarehe 2 Novemba 2022 wakati akifungua Jukwaa la kwanza la watoa huduma wa Sekta ya Posta na Usafirishaji, lilioandaliwa na Shirika la Posta Tanzania kwa kushirikiana na Jumuiya ya Mawasiliano kwa Nchi za Afrika Mashariki (EACO), huku likihusisha Mashirika yote ya Posta kutoka nchi za Afrika mashariki, katika Hoteli ya Mount Meru, Arusha.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape Nnaye (Mb), Mhandisi Kundo ameeleza kuwa jukwaa hilo lenye lengo la kuwakutanisha pamoja wadau wa sekta ya Posta na kubadilishana uzoefu, waangalie namna bora zaidi ya kuboresha huduma za Posta Kwa kuondoa changamoto ndogo ndogo zinazoikumba sekta ya Posta hasa baada ya utandawazi na teknolojia mpya na kujikita kwenye Biashara mtandao na huduma za fedha huduma jumuishi za kifedha Kwa kufanya mabadiliko mahsusi ya kidijitali.

Mhandisi Kundo aliongeza kuwa, jukwaa hilo ni la kwanza kwa Mashirika ya Posta ya Jumuiya hiyo liwe chachu ya kutoa huduma huduma za Posta zilizoboreshwa na kuwafikia wananchi wengi kwa haraka, ufanisi na kwa gharama nafuu kupitia teknolojia za kisasa.

# MHANDISI KUNDO: BORESHENI HUDUMA ZA POSTA ILI ZIANDANE NA MABADILIKO YA TEKNOLOJIA YALIYOKO DUNIANI KWA SASA







"Napenda kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira mazuri na rafiki sana ya kidiplomasia yanayotoa nafasi Kwa taasisi hizi kukutana Kwa uhuru na kujadiliana namna ya kuondoa changamoto mbalimbali zinazowakabili watoa huduma mbalimbali katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, na hii inatokana na namna ambavyo Mh Rais Samia amekuwa kinara wa kuhakikisha mifumo na miundombinu ya mawasiliano nchini inazidi kurahisishwa na kuboreshwa kwa ajili ya maslahi ya wananchi" alisema Mhandisi Kundo.

Vilevile, mhe. Kundo alitumia nafasi hiyo kulipongeza Shirika la Posta Tanzania kwa mabadiliko mengi ya kidijitali ambayo Shirika hilo inayafanya kwa sasa katika huduma zake ikiwemo uwepo wa Posta kiganjani ambayo ni mpya inayounganisha hduma zote za Posta Tanzania kigajanja kwa mteja. Hivyo anajivunia sana kwa Tanzania kupata fursa ya kuandaa jukwaa hilo la kwanza kwa ukanda wa Afrika Mashariki.

Naye Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Mawasiliano ya Afrika Mashariki, Dkt. Ally Yahaya Simba amesema kuwa lengo la jukwaa hilo ni kuinua na kuipa mwelekeo sekta ya Posta ya Afrika Mashariki, kwani kuna fursa nyingi sana kwenye sekta ya usafirishaji, mabadiliko ya kidijitali pamoja na biashara mtandao.

Dkt. Simba amesema kuwa, kupitia Jukwaa hilo wadau wa Sekta ya Posta watapata nafasi ya kuzungumzia namna Sekta ya Posta itakavyosaidia wananchi wake kiuchumi hasa kwa kuzingatia kuwa huduma za kifedha na biashara mtandao ni moja ya majukumu ya Masharika ya Posta.

Aliongeza kuwa, EACO iko katika mchakato wa kuifanya iwe Taasisi Kitovu cha TEHAMA kwa Nchi za Afrika Mashariki ili kuhakikisha yale matunda yanayotokana na Sekta ya Posta yanaonekana na kuwafikia wananchi wa Jumuiya hiyo kwa ufanisi zaidi.

# MHANDISI KUNDO: BORESHENI HUDUMA ZA POSTA ILI ZIANDANE NA MABADILIKO YA TEKNOLOJIA YALIYOKO DUNIANI KWA SASA






Kwa upande wake, Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Ndugu Macrice Mbodo amesema kuwa, ni heshima kubwa kwa Shirika la Posta Tanzania kwa kushirikiana na EACO kuandaa Jukwaa hilo la kwanza kwa Posta za Afrika Mashariki ambalo halikuwahi kufanyika hapo kabla.

"Namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, kupitia mamlaka zake kwa kuturuhusu sisi kuandaa na kufanya mkutano huu. Mageuzi ya Posta yetu ya Tanzania yanayoendelea kufanyika kwa sasa yamekuwa kivutio kwa Posta zingine za Afrika Mashariki na kupitia mkutano huu tutatumia fursa hii kuonyesha namna ambavyo tunatoa huduma zetu kidigitali ili na wenzetu waweze kupata uzoefu kupitia kwetu" Amesema Postamasta Mkuu Mbodo.

Aidha ameeleza kuwa, wameona umuhimu wa kukaa pamoja kama Wakuu wa Posta wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutafakari namna ambavyo Taasisi hizo zitaweza kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia na kushiriki katika mchango wa maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Naye, Katibu Mkuu wa Umoja wa Posta Afrika, Ndugu Sifundo Chief Moyo ameyapongeza Mashirika ya Posta ya Afrika mashariki kwa kuamua kukaa pamoja na kubadilishana uzoefu na mbinu mpya za kuendesha mashirika hayo kwa ufanisi na faida.

Jukwaa hilo la siku tatu, lilihusisha wadau wa Sekta ya Posta na Usafirishaji kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo Wakuu wa Taasisi za Posta kutoka Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Congo, South Sudan pamoja na Wawakilishi kutoka Umoja wa Posta Duniani na Umoja wa Posta Afrika.

# DUKA MTANDAO LA POSTA KURAHISISHA UPATIKANAJI WA BIDHAA KWA WANANCHI



Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Ndg. Macrice mbodo ameeleza namna ambavyo uwepo wa Duka Mtandao la Shirika hilo linavyorahisisha upatikanaji wa huduma pamoja na bidhaa mbalimbali kwa wananchi.

Postamasta Mkuu ameeleza hayo tarehe 08 Oktoba, 2022, wakati alipokuwa akifungua rasmi Kongamano la Biashara Mtandao na Anwani za Makazi ikiwa ni uendelezo wa matukio katika wiki ya maadhimisho ya siku ya Posta Duniani, katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa Kongamano hilo Postamasta Mkuu amesema, Shirika la Posta Tanzania liko tayari kuwahudumia wananchi na kuwafikishia huduma popote pale walipo kupitia Duka hilo kwani mwananchi atawaweza kuagiza chochote na kufikishiwa mpaka mlangoni kwake hususani kupitia uwepo wa Mfumo wa Anwani za Makazi.

"Posta tumeamua kutimiza ndoto ya kila mwananchi ya kupata huduma na bidhaa zake kwa wakati na popote pale walipo kupitia Duka letu la Mtandao ambalo litakuwa limeunganishwa na wadau pamoja na watoa huduma mbalimbali nchini". Amesema Mbodo.

Ameongeza kuwa, maendeleo ya sasa ya teknolojia yanapelekea kubadilika kwa mifumo ya maisha hasa katika masuala ya kibiashara na hivyo kufanya biashara kuhama kutoka analojia na kwenda kidijititali kwa lengo la kurahisisha huduma ziweze kupatikana kwa kasi na ubora Zaidi.

Aidha, Postamasta Mkuu amewataka wadau wanaoshiriki kongamano hilo kutumia fursa hiyo kujadili mahali sasa wananchi walipo na nini kifanyike katika kuboresha huduma za mtandao pamoja na namna ambavyo Mfumo wa Anwani za Makazi unavyowezesha kurahisisha Biashara Mtandao.

Katika hatua nyingine, Ndg. Macrice Mbodo ametumia nafasi hiyo kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuongoza zoezi la uwekaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi ambalo limefanikiwa nchini na sasa imekuwa chachu ya kuboresha miundombinu ya huduma za Posta.

"Tunamshkuru Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake za kuongoza zoezi la Mfumo wa Anwani za Makazi na hatimaye zoezi hilo kufanikiwa kwa asilimia kubwa, huku huduma zetu za Posta zikiwafikia wananchi mpaka mahali walipo".

Naye kwa upande wake Mkurugenzi wa Utawala na Utumishi Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambaye amemuwakilisha Katibu Mkuu Wizara hiyo, Bi. Teddy Njau amelipongeza Shirika la Posta kwa juhudu mbalimbali za kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

"Nawapongeza Shirika la Posta kwa kuendelea kuwafikia wananchi na kurahisisha upatikanaji wa huduma hasa katika kipindi hiki cha maendeleo ya Teknolojia". Amesema Bi. Teddy Njau

Kongamano hilo lilikuwa la siku moja na lina lengo la kuwajengea uelewa wananchi na wadau mbalimbali ikiwemo watoa huduma za mtandao katika kuwahudumia wananchi. Kongamano hilo litahusisha semina mbalimbali ikiwemo Semina ya Biashara Mtandao na Semina ya Mfumo wa Anwani za Makazi.

# TANZANIA NA OMAN YAZINDUA STAMP YA PAMOJA

Tanzania kupitia Shirika la Posta kwa kushirikiana na Posta Oman imezindua Stempu ya Pamoja yenye lengo la kutunza na kuendeleza uhusiano wa kihistoria ulipo baina ya nchi hizi mbili.

Stempu hiyo ya Pamoja kwa nchi hizi mbili imezinduliwa rasmi na Mheshimiwa Nape Nnauye, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Posta Duniani yaliyofanyika katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Uzinduzi huo umehudhuriwa na Naibu Balozi wa Oman Bwana Rashid Al-Manji aliyeongozana na Mtendaji Mkuu wa Posta ya Oman na Asyad Group pamoja na viongozi wengine kutoka Posta Oman.

Aidha, Stempu hiyo imetumia mchoro wa jengo la Maajabu maarufu kama "House of Wonders" lililopo Stone Town, Zanzibar, lengo ikiwa ni kutunza historia ya jengo hili ambalo lina mchango mkubwa kihistoria kati ya nchi hizi mbili.

Ushirikiano huu ambao Taasisi hizi zimefanya ni muendelezo wa ushirikiano unaoendelea kutekelezwa na viongozi wa nchi ya Tanzania na Oman.

Ikumbukwe kuwa Juni, 2022, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan alitembelea nchi ya Oman pamoja na kuona namna ambavyo Posta ya nchini humo inafanya shughuli zake katika kuhudumia wananchi.

Ushirikiano huu ni endelevu na wenye tija katika kuhakikisha wananchi wananufaika na ushirikiano uliyopo, hususani katika huduma mbalimbali zinazotelewa katika nchi hizi hasa katika Sekta ya Posta.









# JUKWAA LA KWANZA LA POSTA NA BIASHARA MTANDAO AFRIKA MASHARIKI

Postamasta Mkuu, aeleza Mafanikio ya Shirika la Posta katika kutoa huduma kidijitali.

Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Ndugu Macrice Mbodo ametoa wasilisho mbele ya Wakuu wa Taasisi za Posta za Afrika Mashariki wakati wa kikao cha tatu cha Jukwaa la kwanza la Posta na Usafirishaji, lililoandaliwa na Shirika la Posta Tanzania (TPC) kwa kushirikiana na Taasisi ya Mawasiliano kwa nchi za Afrika Mashariki (EACO).

Wasilisho hilo limetolewa tarehe 4 Novemba 2022, katika hoteli ya Mount Meru, Arusha ambapo Postamasta Mkuu alieleza namna Posta ilivyopiga hatua ya kutoa huduma kidijitali ikiwemo kuanzisha APP ya Posta Kiganjani ambayo huduma zote za Shirika zitapatikana kiganjani kwa mteja kupitia simu yake ya mkononi au kompyuta Mpakato.

Postamasta Mkuu alieleza namna ambavyo Shirika limepata mafanikio makubwa katika eneo la usafirishaji ikiwemo kumiliki magari makubwa ya hadi tani 30 ambayo yanasafirisha bidhaa mbalimbali ndani na nje ya Nchi ikiwemo Uganda.

Aidha, Postamasta Mkuu alitumia nafasi hiyo kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuliwezesha Shirika la Posta kukua kiteknolojia na kuweka mazingira rafiki ya kidijitali ndani ya Nchi.

Jukwaa hilo la kwanza la Posta na Usafirishaji, limeshirikisha wakuu wa Taasisi za Posta za Nchi Afrika Mashariki, Viongozi wakuu wa Posta Afrika pamoja na Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Umoja wa Posta Duniani,Bwana Mutua Muthusi. Jukwaa hilo linatarajiwa kuhitimishwa leo tarehe 4 Novemba 2022.








# POSTA KUSHIRIKIANA NA NIDA KUSAMBAZA VITAMBULISHO VYA TAIFA



Shirika la Posta Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) limejipanga kimkakati katika kufikisha huduma ya vitambulisho vya Taifa kwa wananchi mahali popote walipo nchi nzima.

Hayo yamebainishwa tarehe 06 Disemba, 2022 wakati wa mazungumzo rasmi baina ya Taasisi hizi mbili yaliyoongozwa na Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Mbodo na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) Bw. Ismail Rumatila katika Makao Makuu ya Posta jijini Dar es Salaam.

Mazungumzo hayo yalilenga kujadili namna bora ya kuwafikishia wananchi huduma ya upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa nchi nzima na hususani katika maeneo ya vijijini kupitia Mfumo wa Posta kiganjani ikihusisha mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi, lengo ikiwa kurahisisha utoaji wa huduma hiyo nchini.

Katika hatua nyingine Mamlaka wa Vitambulisho vya Taifa Tanzania (NIDA) imelipongeza Shirika la Posta Tanzania kwa maboresho ya huduma zake na imeahidi kuendelea kutoa ushirikiano wa kutosha katika kufikisha huduma bora kwa wananchi.

Mazungumzo haya ni muendelezo wa ushirikiano uliopo baina ya Shirika la Posta na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) katika huduma za usafirishaji wa vifurushi vya NIDA na katika kuwahudumia wananchi kupitia vituo vya Huduma Pamoja vilivyopo katika ofisi za Posta.



# MHANDISI KUNDO: USHIRIKIANO WA POSTA KENYA NA POSTA TANZANIA UTAONGEZA FURSA ZA AJIRA NCHINI.




Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Mhandisi Kundo Andrea Mathew (Mb) ameeleza kuwa ushirikiano wa Biashara ya kuvuka mpaka "Cross border business" kati ya Shirika la Posta Tanzania na Shirika la Posta Kenya na uanzishwaji wa vituo maalum vya kubadilishana mizigo Kimataifa "Office of Exchange" utapunguza muda wa usambazaji na gharama za usafirishaji wa barua, vifurushi na Mizigo ya wateja pamoja na kuongeza fursa za Ajira.

Mhe. Kundo ameyasema hayo tarehe 01 Novemba, 2022 akimwakilisha Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Moses Nnauye aliyekuwa Mgeni Rasmi wa hafla ya Uzinduzi wa biashara ya kuvuka mpaka kati ya Shirika la Posta Tanzania na Shirika la Posta Kenya, kwenye mpaka wa Namanga Wilayani Longido.

"Gharama za usafirishaji na mizunguko mirefu ya vifurushi vya Wananchi kati ya Nchi hizi mbili unakwenda kupungua, lakini pia kutokana na kuanzishwa kwa vituo vya pamoja vya ubadilishanaji wa mizigo nimeona ziko fursa za ajira zinaenda kupatikana kwa watanzania" alizungumza Mhandisi Kundo.

Aidha Mhe. Kundo alieleza kuwa ushirikiano huu utaondoa usumbufu mkubwa uliokuwepo hapo awali, ambapo mteja anayetuma barua au kifurushi kutoka hapa Namanga, Arusha kwenda Nairobi, Kenya ilimlazimu kifurushi chake kurudi Dar es Salaam kwa ajili ya mchakato wa usafirishaji, kisha kitoke Dar es Salaam na kusafirishwa kwenda Nairobi, Kenya. Hivyo uwepo wa vituo hivi utapunguza mzunguko mrefu wa vifurushi vya wateja kwa kuwa mizigo itatoka Arusha moja kwa moja kwenda Nairobi.

Katika hatua nyingine Naibu Waziri Kundo ametumia nafasi hiyo kulipongeza Shirika la Posta nchini kwa jitihada zake za kukuza mahusiano mazuri na Posta nyingine duniani huku akipongeza Shirika hilo kwa hatua kubwa ya ushirikiano huo wenye lengo la kurahisisha huduma za posta na usafirishaji.

Naye, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Ndugu Mohammed Abdulla amesema kuwa, Shirika la Posta ndio msingi wa Mawasiliano na Usafirishaji Nchini. Hivyo ushirikiano huu utazidi kuimarisha sekta ya usafirishaji na kurahisisha maisha ya wananchi.

Vilevile, Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro Ndugu Raymond Mangwala amelipongeza Shirika la Posta Tanzania na Shirika la Posta Kenya kwa ushirikiano huo wenye tija kwa wananchi na Taifa huku akilitaka Shirika la Posta kupanua wigo wa biashara mtandao.

Kwa upande wake, Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Ndg. Macrice Mbodo ameeleza namna ambavyo Shirika hilo linavyoendelea kuboresha huduma zake za usafirishaji na Teknolojia ili kuwapunguzia wananchi adha ya kupata huduma za Posta pale wanapohitaji, huduma hizo mahali popote walipo. Aidha Postamasta Mkuu alimeongeza kuwa Shirika linaendelea na mageuzi ya kidijitalli ili kukuza ufanisi zaidi wa huduma zake.

Aidha, Uzinduzi huo ulihudhuriwa na Mwakalishi wa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia Kenya, Ndugu Paul Macharia, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Posta Tanzania, Brigedia Jenerali Mstaafu Yohana Ocholla Mabongo na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Posta Kenya Ndugu Peter Kanaiya na Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Kenya ndugu Dan Kagwe.



# MATUKIO KATIKA PICHA WAKATI WA HAFLA YA UZINDUZI WA BIASHARA YA KUVUKA MPAKA KATI YA SHIRIKA LA POSTA TANZANIA NA SHIRIKA LA POSTA KENYA









# POSTA ZA AFRIKA MASHARIKI, ZAJIDHATITI KUTOA HUDUMA KIDIJITALI




Wadau wa huduma za Posta na Usafirishaji kutoka nchi za Afrika Mashariki wamekutana na kujadiliana namna mashirika ya Posta ukanda wa Afrika Mashariki yanavyoweza kushirikiana na Mamlaka za Mawasiliano pamoja na watunga Sera kutoka nchi zao katika kukabiliana na mabadiliko ya kidijiti hususani katika sekta ya usafirishaji, biashara mtandao na huduma za kifedha.

Majadiliano hayo yamefanyika tarehe 3 Novemba, 2022 ambapo Tanzania kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) pamoja na Kenya kupitia Mamlaka yake ya Mawasiliano Kenya (CA) walitoa mawasilisho ya namna ambavyo Taasisi hizo zinavyosaidia kudhibiti mawasiliano na ukuaji wa sekta ya Posta na usafirishaji ndani ya nchi zao, jijini Arusha.

Aidha, Dkt. Emmanuel Manasseh aliyemwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), alitoa wasilisho lililoeleza namna ambavyo Mamlaka hiyo inadhibiti uhalifu wa mitandao pamoja na kufuatilia kwa karibu utoaji wa taarifa mitandaoni, usalama wa matumizi ya fedha mtandao, pamoja na Biashara mtandao zinazofanywa na watu binafsi na Taasisi likiwemo Shirika la Posta Tanzania.

Naye, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Kenya (CA), Ndg. Bernard Nderitu alieleza namna Mamlaka hiyo inavyoshirikiana na Shirika la Posta Kenya katika kuleta mabadiliko chanya ya teknolojia ya mawasiliano, biashara mtandao na huduma jumuishi za kifedha.

Sambamba na mawasilisho hayo, baadhi ya Wakuu wa Taasisi za Posta za ukanda wa Afrika Mashariki walipata fursa ya kueleza namna ambavyo Posta katika nchi zao zilivyoweza kupiga hatua katika katika matumizi ya TEHAMA hasa katika huduma za Posta, huku lengo likiwa kurahisisha upatikanaji wa huduma wa wananchi kulingana na mahitaji yao.



Nchi zilizopata fursa ya kuwasilisha ni pamoja na Rwanda na Burundi ambapo Postamasta Mkuu wa Posta Burundi Bi. Le'a Ngabire alizungumzia namna Shirika hilo linavyotumia mitandao katika kurahisisha huduma za malipo watumiaji wa huduma za Posta nchini humo

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Posta Rwanda, Ndg. Celestine Kayitare alieleza namna Shirika hilo lilivyoandaa mradi wa mabadiliko ya kidijitali uitwao "Kuwezesha kesho yako" (Enabling the future project), huku wakitarajia kuanzisha maghala na vituo vya biashara mtandao kutokana na kuwa na mifumo mizuri ya Anwani za wateja.

Jukwaa la kwanza la Posta na Usafirishaji limekuwa na kikao chake kwa siku mbili huku likihudhuriwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Posta Afrika, Ndugu Sifundo Chief Moyo, Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Ndg. Macrice Mbodo na Wakuu wa Mashirika ya Posta pamoja na wawakilishi kutoka Posta za Afrika Mashariki, Umoja wa Posta Afrika na Umoja wa Posta Duniani.

# UMOJA WA POSTA DUNIANI KUENDELEA KUTOA USHIRIKIANO KWA TANZANIA




**Taasisi za Posta zatakiwa kutumia fursa za maendeleo ya kidijiti**

Yaahidi kuweka mikakati madhubiti ya kuwezesha matumizi TEHAMA kwenye sekta ya Posta duniani

Mkurugenzi wa Maendeleo na Ushirikiano wa Umoja wa Posta Duniani(UPU) Bw. Mutua Muthusi, akimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa Umoja huo Bw. Masahiko Metoki ameahidi kuendelea kuwezesha Sekta ya Posta katika kusambaza huduma zake kimataifa.

Ameyasema hayo tarehe 05 Novemba, 2022, wakati alipofanya ziara yake Makao Makuu ya Shirika la Posta Tanzania, jijini Dar es Salaam.

Lengo la ziara hii ni kutembelea na kukagua ofisi ya Mtaalamu wa Miradi wa Umoja wa Posta Duniani kwa Ukanda wa Afrika Mashariki zilizopo katika Makao Makuu ya Shirika la Posta Tanzania, jijini Dar es Salaam.

Katika ziara yake Bw. Muthusi, ameeleza kuwa Mashirika ya Posta Duniani yanapaswa kutumia fursa ya maendeleo ya kidigitali katika kuboresha huduma zake ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

Aidha, ametumia nafasi hiyo kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Uongozi wa Rais wake Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya kidigitali katika Tanzania huku ikilirahishia Shirika la Posta Tanzania kutoa huduma zake sambamba na mahitaji ya wananchi.

Katika hatua nyingine, Mkurugenzi wa Ushirikiano wa Maendeleo Bw. Mutua Muthusi, ametembelea Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo Bw. Bakari Jabiri, katika mazungumzo yao ameipongeza Mamlaka hiyo kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuwezesha Mawasiliano nchini hususani katika Sekta ya Posta.

Itakumbukwa kuwa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Shirika la Posta Tanzania imepewa heshima na Umoja wa Posta Duniani ya kuanzisha Ofisi za Umoja wa Posta Duniani kwa Ukanda wa Afrika Mashariki pamoja na kutoa Mtaalamu wa Kuratibu Miradi kwa Ukanda huo (UPU Field Project Expert for East Africa Sub-Region).

# MBODO: "KIKAO CHENU KIJIKITE KUJADILI MWELEKEO WA POSTA KUFANYA HUDUMA ZAKE KIDIJITALI"



Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Mbodo ameliasa Baraza la Majadiliano la Shirika hilo lijikite kujadili mikakati ya kuendelea kuboresha utoaji wa huduma za Posta kidijitali ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wateja na wananchi kwa ujumla pamoja na kuongeza mapato.

Ameyasema hayo tarehe 9 Novemba, 2022 wakati akifungua kikao cha 34 cha Baraza la Majadiliano cha Shirika la Posta Tanzania katika ukumbi wa mikutano wa hoteli ya Adden Palace, Jijini Mwanza.

Akizungumza wakati wa kikao hicho, Postamasta Mkuu amewaasa Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi na Wafanyakazi wa Shirika hilo kubadili mitazamo yao katika utendaji kwani kwa sasa wananchi wanataka kuhudumiwa wakiwa mahali walipo, hii ni kutokana na kasi ya mabadiliko ya kiteknolojia na vionjo vya wateja kulingana na maendeleo ya kidijitali.

"Miaka 20 iliyopita sio kama sasa kwa sababu kwa sasa wananchi wanataka kuhudumiwa wakati wowote na mahali popote kwa kasi na weledi zaidi kwani wananchi wanataka kufuatwa mpaka walipo". Akisisitiza Bw. Mbodo.

Aidha Postamasta Mkuu ameeleza kuwa, Menejimenti ya Shirika la Posta kupitia mpango mkakati wake wa 8 wa Shirika hilo imedhamiria kuifanya Posta ya Kidijitali kwa Biashara Endelevu ili kuendana na mikakati na agenda mbalimbali za kitaifa na kimataifa katika kutoa huduma stahiki kulingana na mahitaji ya wateja.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Baraza la Majadiliano ndugu Bw. Omari M. Dibibi Amempongeza Postamasta Mkuu Bw. Macrice Mbodo kwa juhudi zake na maono ya kuifanya Posta kuwa ya kidijitali na pia amemuahidi kuunga mkono juhudi hizo za kimaendeleo zinazofanywa na Shirika ili kuleta matokeo chanya yenye tija kwa Shirika.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Baraza hilo Bw. Mbaruku Makame ametumia nafasi hiyo kuwataka Wafanyakazi wa Shirika la Posta Tanzania kufuata misingi ya kazi na kuunga mkono maono ya Shirika yaliyomo kwenye mpango mkakati wa 8 kama ilivyofafanuliwa na Postamasta Mkuu wa Shirika hilo.

# MENEJIMENTI YA SHIRIKA LA POSTA TANZANIA YAPITISHWA KWENYE MUUNDO NA MWONGOZO WA HUDUMA PAMOJA



Menejiment ya Shirika la Posta Tanzania tarehe 23 Novemba 2022 imepata nafasi ya kupitishwa kwenye muundo wa Biashara Pamoja na mwongozo wa ufanyaji kazi wa Vituo vya HUDUMA PAMOJA unaoandaliwa na Mtaalaam Mwelekezi kutoka Kampuni ya UNIX ya jijini Dar es Salaam.

Katika kikao hicho, Mtaalam mwelekezi alieleza namna mtindo wa Biashara " business model" hiyo pamoja na mwongozo wake utavyokuwa rafiki na wenye kuwezesha wananchi kupata huduma wanazozihitaji pasipo usumbufu wa aina yoyote na kupelekea kufaidisha Serikali, Pia Shirika la Posta Tanzania na wadau wote wakiwemo wananchi watakaokuwa wanahudumiwa na Vituo vya HUDUMA PAMOJA nchi nzima kupitia ofisi za Posta.

Hata hivyo, taarifa hiyo ililenga zaidi kuielewesha Menejimenti ya Shirika kama mdau muhimu juu ya namna ya muundo na mwongozo wa Vituo vya HUDUMA PAMOJA utakavyokuwa ikiwa ni pamoja na mpango kazi utakaopelekea kutekelezwa kwa ufanisi kwa uanzishwaji na ufanyaji kazi wa vituo hivyo nchi nzima.

Aidha, Timu ya watalaam welekezi kutoka Unix iliongozwa na Mhandisi Ndg. Gerald P Malima ambaye ni Meneja wa Mradi akiambatana na Pauline Mtunda Meneja Mshauri Mkuu, Emmanuel Kanagisa Kiongozi wa timu,Pamoja na Adv. Vedastus Majura Mtaalamu wa Sheria, ambapo Menejimenti ya Shirika la Posta Tanzania ikiongozwa na Kaimu Postamasta Mkuu Ndg.Constantine Kasese pamoja na menejimenti ya Shirika hilo.



Bidhaa na huduma za Shirika la Posta Tanzania zimegawanyika katika makundi Nane (8) kama ifuatavyo:-

## 01. USAFIRISHAJI WA KAWAIDA

Kundi hili linahusisha usafirishaji ambao hupokea (Accept), husafirisha (Convey), na kusambaza (deliver) Barua, Vipeto, Mizigo na Vifurushi kwa njia ya kawaida kupitia njia ya maji na nchi kavu (meli, barabara na reli):

### Barua za Kawaida:

Hizi ni barua zisizozidi uzito wa kilogramu mbili (2kg), kwenda ndani na nje ya nchi. Barua hizi zinatakiwa kuwekwa Anwani ya mtumiwa kwa mbele na Anwani ya mtumaji kwa nyuma. Hata hivyo barua hizi haziwekwi alama/ namba ya ufuatiliaji (tracking number).
Barua za aina hii zinaweza kulipiwa kwa gharama nafuu (economy mail) au gharama za kupewa kipaumbele (priority mail)

### Rejesta

Hizi rejesta hazizidi uzito wa kilogramu mbili (2kgs). Ili iitwe rejesta lazima iwekwe namba maalum ya ufuatiliaji (tracking number) yenye kuanza na neno RD na kuishia na neno TZ kwa rejesta za ndani au RR na kuishia na neno TZ kwa rejesta za kimataifa. Barua za aina hii huashiria kuwekwa vitu vya thamani ndani yake kama hati, vyeti, nk.

### Vipeto

Vipeto vina tofauti na barua za kawaida kwa kuwa huwa na vitu vya thamani ndani mwake na kufungwa kama kifurushi kidogo chini ya kilo tatu (3Kgs). Huwekwa namba maalum ya ufuatiliaji (tracking number) kwa mtiririko wa vipeto.

### Vifurushi vya kawaida

Vifurushi vya kawaida huanzia uzito unaozidi kilo 3 hadi kilo 30. Huwekwa namba maalum ya ufuatiliaji (tracking number) kwa vifurushi vya nchini na vya kimataifa. Vifurushi vya kimataifa lazima vifungwe mbele ya afisa wa Posta na maafisa Ushuru wa Forodha ili kuorodhesha kwa uhakika vitu vilivyofungwa ndani ya kifurushi. Kufanya hivi husaidia kujaza fomu ya kiapo (declaration form) inayoambatana na kifurushi husika ili kifurushi kitakapofika nchi kinapokwenda mteja aweze kukadiriwa ushuru wa forodha kwa urahisi.



### Mifuko ya Barua (M- Bag):

Huduma hii ni ya kusafirisha mizigo kwenye mfuko maalum kwa lengo la kurejesha au kutanguliza mizigo ya mtu aliyekwenda kwa shughuli maalum nje ya nchi yake.

### Posta Mlangoni

Barua za posta mlangoni hupelekwa kwa kawaida na barua kufikishwa hadi nyumbani kulingana na Anwani za Makazi. Hivyo barua, nyaraka na vifurushi vya wateja kutoka ndani na nje ya nchi na husafirishwa na kufikishwa hadi nyumbani au ofisini kwa gharama nafuu kwa kutumia Anwani za Makazi na Postikodi.

### Mizigo ya Posta (Post Cargo)

Ni huduma maalum kwa ajili ya usafirishaji mizigo yenye uzito mkubwa zaidi ya kilogram 30 au yenye umbo lisiloweza kufungwa kama kifurushi na kutumwa Posta. Huduma hii ni nzuri kwa wateja wenye mizigo ya aina hii na wanaohamisha mizigo mikubwa kama samani za ndani, nafaka, biashara, nk

### Nyaraka au maandishi kwa wasioona

Shirika hutoa huduma maalum kwa wateja wanaotuma au kutumiwa nyaraka au maandishi kwa wasioona (literature for the blind). Huduma hii ni bure. Hii ni kutokana na mkataba maalumu wa Umoja wa Posta Duniani kuwa nyaraka hizi zisafirishwe bure na Posta zote teule(designated postal Operators) za Serikali.

## 02. USAFIRISHAJI WA HARAKA

Kundi hili linahusisha usafirishaji ambao hupokea (Accept), husafirisha (Convey), na kusambaza (deliver) Nyaraka, Vipeto na Vifurushi kwa njia ya haraka ambao hufanywa kwa ndege au usafiri wa haraka uliopo kutegemea na maeneo. Usafirishaji huu hufanyika kwenye huduma zifuatazo:

### Nyaraka za EMS

Ni huduma ya kusafirisha na kusambaza nyaraka na vipeto muhimu kwa haraka na usalama ndani na nje ya nchi kwa malipo yanayowezesha kufikishwa hadi nyumbani. Kila nyaraka ya EMS huwekwa namba maalum ya ufuatiliaji (tracking number) yenye kuanza na neno EE na kuishia na neno TZ kwa huduma hii mpokeaji hutakiwa kusaini ili kuthibitisha amepokea nyaraka husika.

### Vifurushi vya EMS

Ni huduma ya kusafirisha na kusambaza vifurushi kwa haraka na usalama ndani na nje ya nchi kwa malipo yanayowezesha kufikishwa hadi nyumbani. Kila kifurushi cha EMS huwekwa namba maalum ya ufuatiliaji (tracking number) yenye kuanza na EE na kuishia na neno TZ kwa huduma hii Mpokeaji hutakiwa kusaini kuthibitisha kuwa kifushi chake kimepokelewa.

### Barua za Haraka kwenye Miji (Posta City Urgent Mail-pCUM)

Ni huduma ya kusafirisha barua, virufushi na nyaraka ndani ya miji au jiji kutoka kwa mteja na kupelekwa moja kwa moja kwa mteja anayetakiwa kupokea pasipo kupitisha kuchakatwa kwenye ofisi za Posta.

### Usambazaji wa Sampuli za Maabara

Shirika la Posta limepewa jukumu na Wizara ya Afya ili kupokea, kusafirisha na kufikisha sampuli za maabara kutoka kwenye vituo vidogo na kupelekwa maabara kwa ajili ya vipimo na kurudisha majibu kwa haraka. Huduma hii husaidia wananchi kupata majibu ya vipimo kwa wakati.

## 03. FEDHA NA UWAKALA

Huduma ya Fedha na Uwakala hufanyika kwa ajili ya wananchi kuwawezesha kupata huduma mbalimbali za kifedha na nyingine za aina hiyo zinazotolewa na Shirika kwa njia ya Uwakala. Huduma hizi ni kama ifuatavyo:




### Posta Keshi (Posta Cash)

Posta keshi ni jukwaa la upokeaji, usafirishaji na ulipaji wa fedha kutoka kwa mteja mmoja Kwenda kwa mwingine. Huduma hii hutolewa kwa wateja wa ndani ya nchi. Huduma hii ni miongoni mwa huduma zitolewazo kupitia katika mfumo wa Posta Kiganjani. Huduma hii ni ya gharama nafuu, hulipwa kupitia simu za mkononi, inaweza kupokelewa kwenye mtandao wowote wa simu, na mteja anaweza kutuma au kupokea fedha katika ofisi za Posta au kwa Wakala yeyote wa Posta aliyesajiliwa.

### Giro ya Posta (Post Giro)

Giro ya Posta ni huduma ya kulipa kwa niaba ya mteja. Mteja anaweza kutuma au kulipa au kupokea fedha kupitia mfumo huu wa malipo. Aidha, mteja anaweza kununua au kuuza hisa kupitia mfumo huu. Malipo yanayoweza kulipwa ni pamoja na:

- Mafao ya uzeeni (pensheni),
- Mishahara ya watumishi,
- Ada za shule,
- Kuuza na kununua hisa za makampuni yaliyosajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam,
- Mafao ya Bima,
- Malipo ya gawio litokanalo na uwekezaji wa Hisa,
- Kodi mbalimbali na
- Ankara mbalimbali kama za maji na umeme.

### Usafirishaji Fedha:

Shirika hupokea na kulipa wateja wake kupitia mifumo mbalimbali ya malipo ikiwemo Western Union, Money Gram kwa njia ya Uwakala

- Huduma za Mabenki: Shirika ni Wakala wa utoaji wa huduma za kibenki zikiwemo za Benki ya CRDB, TCB, NBC, PBZ na Equity Bank.

- Huduma za Bima: Shirika hutoa huduma za Bima kwa uwakala kwa NIC, ZIC na Assemble Insurance.

- Huduma za Simu: Shirika linatoa huduma mbalimbali za uwakala kwa Makampuni ya simu ya TTCL (T-Pesa), Vodacom (M-Pesa), Tigo (Tigo Pesa), na Halotel (Halo Pesa)

## 04 DUKA LA KUUZA NA KUNUNUA FEDHA ZA KIGENI

Huduma ya kubadilisha (kuuza na kununua) fedha za kigeni hutolewa kupitia maduka ya kubadilisha fedha za kigeni ya Posta. Gharama zake ni za ushindani kulingana na hali ya soko. Tunajivunia kutoa viwango bora vya ubadilishaji wa fedha za kigeni kwa wateja wetu.

Huduma hizi zinapatikana kwenye matawi yafuatayo:

- Mkoa wa Dar es Salaam: Posta Kuu DSM, Airport Termina II na III, Posta ya Libya, Posta ya Kariakoo, Posta ya Oysterbay, Posta ya Kijitonyama na Posta ya Sokoine.
- Mkoa wa Arusha: Posta Kuu Arusha, Posta ya Namanga, Posta ya Karatu.
- Zanzibar: Posta Kuu Zanzibar, Zanzibar Airport na Posta ya Kijangwani.
- Mkoa wa Kilimanjaro: Kilimanjaro Airport na Posta ya Marangu-Moshi.
- Mkoa wa Kigoma: Posta Kuu Kigoma (HPO) na Posta ya Kasulu.
- Mkoa wa Mwanza: Posta Kuu Mwanza (HPO) na Mwanza Airport.
- Mkoa wa Mbeya: Posta Kuu Mbeya (HPO) na Posta ya Tunduma
- Mkoa wa Morogoro: Posta Kuu Morogoro (HPO)
- Mkoa wa Dodoma: Posta Kuu Dodoma (HPO).

## 05. BIASHARA MTANDAO

Biashara mtandao ni huduma za kidijitali zinazotolewa na Shirika kwa ajili ya kukuza na kuimarisha biashara za wajasiriamali na makampuni yanayotaka kufanya biashara mtandao.

Biashara mtandao ipo kwenye Duka Mtandao la Posta, Uuzaji wa Stempu mtandaoni na Uuzaji wa Stempu za maonesho (philatelic stamps) mtandaoni.

Upatikanaji wake ni wa kidijitali kupitia njia zifuatazo:

- **Duka mtandao kupitia www.postashoptz.post**

Ni huduma ya kuuza, kununua na kutangaza bidhaa na huduma mbalimbali za wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo na wakubwa kwa njia ya mtandao wa pamoja ulioanzishwa na Shirika la Posta Tanzania na duka hili limeunganishwa na linapatikana kwenye nchi 192 duniani zilizopo chini ya umoja wa Posta duniani (UPU). Duka hili linatumia lugha zaidi ya 20 ambazo hutumika kuwasiliana na mataifa mbalimbali. Mfanyabiashara/mjasiriamali anaweza kujisajili kupitia tovuti www.postashoptz.post. Duka hili limekuwa msaada mkubwa sana kwa wajasiriamali katika kukuza biashara zao kwa kuwafikia wateja wengi duniani.

- **Uuzaji wa Stempu mtandaoni**

Uuzaji wa stempu hufanyika posta au mtandaoni ambapo hupatikana kwenye duka mtandao www.stemps.tz.post. na mnunuzi kupelekewa mahali alipo. Stempu ni bidhaa ambayo huwakilisha mambo matatu: Bidhaa, Gharama za Usafirishaji na Balozi wa Nchi. Huonesha utalii wa nchi, uchumi wa nchi, shughuli za kijamii, historia, vipaji (talents) vya wananchi, nk.

Aidha, Stempu huonesha maeneo ya urithi, wanyama, mimea, mbuga za wanyama, watu maarufu n.k. ambayo hulipwa fedha sawa na kiasi kinacholingana na thamani yake kabla haijatumiwa katika barua au nyaraka.

- **Uuzaji wa Stempu za wakusanyaji/maonesho mtandaoni (e-philatelic stamps)**

Ni huduma ya kuuza stempu za mtandaoni kupitia duka linalopatikana kupitia tovuti www.stamps.tz.post. Wanunuzi/ wakusanyaji (stamp collectors) wanaweza kuonesha au kuuza stempu kwa wateja wengine.

Ukusanyaji wa stempu ni sehemu ya utafiti wa stempu za posta, alama za posta na nyenzo zinazohusiana na hizo. Ukusanyaji wa stempu ni shauku ya kielimu sana, inahusisha mkusanyiko wa stempu na utunzaji wa stempu za miaka mbalimbali kwa mpangilio mzuri.

Ukusanyaji wa stempu umekuwepo kwa miaka mingi, ilikuwa ni lazima mtu atumie pesa kununua, kubadilishana au kupata stempu za matoleo mbalimbali. Leo wakusanyaji wanaweza kuuza stempu hizo kwa bei ya juu sana kwenye soko la philatelic stamps. Ukusanyaji wa stempu bado hubaki kuwa ni tabia ya kurithisha kwa mkusanya stempu mwenyewe.

**• Huduma ya vituo vya Intaneti (Internet Café)**

Ni huduma inayotolewa kwa wateja wanao hitaji huduma za mtandao kupitia intaneti zilizo katika ofisi za Posta. Huduma zitolewazo ni kudurufu nyaraka na zingine kama kuchapisha, kusambaza na kuvinjari mtandaoni (Printing, Scanning, Surfing/ Browsing).

**• Sanduku la kielekitronic (Virtual Box)**

Ni huduma ya kumiliki sanduku la kielekitronic kwa njia ya mtandao, ambapo mteja atasajili namba yake ya simu kuwa sanduku la Posta kwa kutumia simu ya mkononi, kishkwambi au kompyuta mpakato (Laptop). Huduma hii inapatikana kupitia mfumo wa Posta Kiganjani.

**Mteja anaweza kujisajili kama:**

- Mtu binafsi (Individua customer). Kujisajili ni Tsh.14,160/=
- Kampuni (Corporate customer). Kusajili gharama yake ni Tsh.59,000/=

Mteja atajisajili kupitia "Appstore", "Playstore", Postawebsite: www.posta.co.tz au link: https://postakiganjani.posta.co.tz.

## 6: UPANGISHAJI NA MILIKI (REAL ESTATE).

Shirika limamiliki viwanja wazi na majengo kwa ajili ya kupangisha ofisi na nyumba za kuishi katika mikoa mbalimbali nchini:

- Hukodisha kumbi kwa ajili ya matukio na mikutano katika mikoa mbalimbali.
- Maeneo ya kuegesha magari ya watu binafsi na taasisi kwa bei nafuu sana.
- Hupangisha maeneo ya kuweka mabango ya matangazo na kusimika minara ya mawasiliano.

## 7. VITUO VYA HUDUMA PAMOJA

Serikali ina lengo la kuboresha utoaji wa huduma zake kwa kuwapunguzia wananchi muda mrefu na gharama za kutafuta huduma hizo. Hivyo Serikali imeanzisha Vituo vya Huduma Pamoja vinavyowezesha upatikanaji wa huduma za Serikali katika eneo moja ndani ya majengo ya Ofisi za Shirika la Posta Tanzania. Lengo kuu ni kufanya maboresho na mageuzi katika utoaji huduma kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano baina ya Taasisi za Serikali.

Huduma zitolewazo kwenye vituo vya Huduma Pamoja kwa sasa ni:-

- Vyeti vya kuzaliwa na kifo - RITA;
- Utoaji wa Pasipoti-UHAMIAJI;
- Utoaji wa Kitambulisho cha Taifa-NIDA;
- Usajili wa kampuni za Biashara-BRELA;
- Utoaji wa Namba ya Mlipa Kodi (TIN)-TRA;
- Taarifa za pensheni ya uzeeni, kujisali, uhakiki taarifa-PSSSF&NSSF; na
- Utoaji wa Taarifa ya mali iliyopote na uhakiki kwa ajili ya kupata leseni za udereva – Jeshi la Polisi Tanzania TPF.
- Utoaji wa Leseni za Biashara za Halmashauri ya Jiji Dodoma

## 8.UWEKEZAJI BENKI YA TAIFA YA BIASHARA (TCB) BANK

Shirika la Posta ni mwekezaji kwenye Benki ya Taifa ya Biashara tangu mwaka 1992. Wakati huo Shirika la Posta na Simu yalikuwa pamoja na Benki ya Posta. Baada ya kutengana Shirika lilikuwa linamiliki asiliamia 30% lakini kutokana na kutoendelea kuweka limebakia na 7% ambayo ni sawa na Tshs.....Hii hulipatia Shirika mgao wa faida.



# SHIRIKA LA POSTA LAWAKUMBUKA MASHUJAA WA VITA YA KWANZA YA DUNIA



Tarehe 13 Novemba 2022 Shirika la Posta Tanzania likiwakilishwa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Mahusiano ya Posta Kimataifa, Ndugu Elia Madulesi kwa niaba ya Postamasta Mkuu, limeweka Shada la maua kwenye jengo la Posta ya Zamani (Sokoine) kama ishara ya kuwakumbuka baadhi ya *Wafanyakazi wa Posta na Simu* wa iliyokuwa Serikali ya kikoloni ya Ujerumani na Uingereza, waliokufa wakati wa Vita kuu ya Kwanza ya dunia.

Wafanyakazi hao waliokuwa wataalamu wa mifumo ya Mawasiliano ya Posta na simu, walihusika kama wadukuzi na watoa taarifa za vita, huku wakifanya kazi katika Jengo la Posta Sokoine ambalo ndilo lililokuwa Makao Makuu ya Posta na Simu ya Serikali za kikoloni katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Uwekaji huo wa mashada umehusisha baadhi ya Wafanyakazi kutoka Shirika la Posta Tanzania, wawakilishi kutoka Ubalozi wa Uingereza, Ubalozi wa Ujerumani, na Jumuiya ya Mashujaa wa Uingereza.





# DKT. JIM YONAZI AFUNGUA KIKAO CHA KWANZA CHA KUANZA UPEMBUZI YAKINIFU (FEASIBILITY STUDY) KUHUSIANA NA UJENZI WA KITUO CHA BIASHARA ZA KIMTANDAO (E-COMMERCE HUB)



Katibu Mkuu, Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Jim Yonazi amefungua kikao cha kuanza Upembuzi Yakinifu(Feasibility Study) kwa ajili ya ujenzi wa maghala ya kuhifadhia bidhaa za biashara mtandao jijini Dar es salaam tarehe 15 Disemba,2022.

Kikao hiki kilichofanyika kwa siku mbili kuanzia tarehe 15-16 Disemba,2022 ni mwendelezo wa utiliwaji saini makubaliano ya Ushirikiano wa kibiashara(MoU) baina ya Posta ya Tanzania na Oman hivi karibu jijini Muscat, Oman ambapo Posta masta Mkuu Bw. Macrice Mbodo na mwenzake wa Oman Bwana Nasser Al-Sharji walitiliana saini kushirikiana wakishuhudiwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Ikumbukwe kuwa makubaliano kati ya Mashirika hayo mawili yanalenga kupanua wigo kwa upande wa masoko kwa kuendeleza ushirikiano na mataifa mbalimbali duniani huku ikidhamiria kukuza biashara za mipakani na kuongeza wigo wa biashara za mtandao ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi wanapokuwa mahali popote Tanzania ambapo kupitia Shirika la Posta itakua na eneo maalum (Maghala) litakalotumika kuhifadhi bidhaa na shughuli za Biashara Mtandao sambamba na vitendea kazi vya kisasa ili kurahisisha huduma hiyo nchini.

Vilevile Shirika la Posta linatazamiwa kupata soko kubwa la biashara mtandao kutoka Oman na Nchi zote kupitia maduka makubwa duniani ambapo mizigo mingi hususani kwa ukanda wa Afrika mashariki itapitia nchini na hii itaongeza pato la Shirika na la Taifa kwa ujumla.

TPC iliwakilishwa na Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice D. Mbodo pamoja na viongozi waandamizi wa ShirikaMtendaji Mkuu wa Posta Oman pamoja na wataalamu wake, Wataalamu kutoka Kampuni ya ALG Transport & Infrastructure ambayo ndiyo iliyoshinda zabuni ya kufanya upembuzi yakinifu.

Upembuzi yakinifu huo unatarajia kudumu kwa kipindi cha miezi mitatu na baada ya hapo matokeo yatakayopatikana ndiyo yataamua mwelekeo wa uwekezaji kwenye mradi huo.

# POSTA YASHIRIKI MAONESHO YA SABA YA BIDHAA ZA VIWANDA








Shirika la Posta Tanzania linashiriki maonesho ya Saba ya bidhaa za viwanda yaliyofunguliwa rasmi tarehe 4 Disemba, 2022 na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Omar Said Shaaban.

Maonesho hayo yenye kauli mbiu isemayo "Nunua Bidhaa za Tanzania Jenga Tanzania; Nunua cha kwetu" yanafanyika katika viwanja vya Sabasaba, lengo likiwa ni kutangaza bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na kutengenezwa na Viwanda vikubwa na vidogo hapa nchini.

Katika hotuba yake, Mhe. Omar Shaaban aliwataka wenye viwanda kuongeza ubora wa bidhaa na kasi ya uzalishaji ili kuweza kuzalisha bidhaa zitakazokidhi matakwa ya kimataifa na hatimaye kupata masoko ya haraka ndani na nje ya nchi yatakayokuza vipato binafsi na Taifa kwa ujumla.

"Washiriki wa maonesho haya tunawategemea sana muongeze ubora wa bidhaa na kasi ya uzalishaji ili bidhaa zenu zikidhi matakwa ya Kimataifa na kipato cha mtu mmoja mmoja na Taifa" alielekeza Mhe. Omar.

Aidha Mhe. Shaaban alieleza kuwa kutokana na mazingira wezeshi na rafiki ya viwanda yaliyowekwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ndio yakiyopelekea mwaka huu maonesho hayo kupata Washiriki 502 kati ya Washiriki 121 pekee waliokuwepo katika Maonesho hayo mwaka jana.

Shirika la Posta lilishiriki maonesha hayo kama mdau muhimu wa Shughuli za Viwanda kwa kutoa huduma za Biashara Mtandao kupitia Duka Mtandao la Posta liitwalo "Posta Online Shop". Duka lililounganishwa na Nchi 192 zilizoko kwenye Umoja wa Posta Duniani, linatoa fursa ya viwanda vya Tanzania kutangaza na kuuza bidhaa zao bure hivyo kuongeza masoko mapya Kitaifa na Kimataifa.

Aidha, huduma nyingine zilizokuwa zinatolewa na Shirika la Posta katika maonesho hayo ni pamoja na huduma za Usafirishaji wa Mizigo Mikubwa "Post Cargo", huduma ya usafirishaji wa Haraka "EMS" na Huduma ya Sanduku la Posta la kidijiti "Virtual Box".

Maonesho hayo ya bidhaa za viwanda yanatarajiwa kumalizika tarehe 9 Disemba 2022.




# TANZANIA YASAINI MAKUBALIANO YA USHIRIKIANO WA KIBIASHARA (MoU) NA POSTA OMAN.

Tarehe 24 Novemba, 2022 Tanzania kupitia Shirika la Posta Tanzania limesaini makubaliano ya kibiashara na Shirika la Posta Oman (Asyad Group) katika Biashara Mtandao lengo likiwa ni kupanua wigo wa kimataifa wa Biashara Mtandao Uli kuiwezesha Tanzania kuwa kitovu cha Biashara Mtandao kwa ukanda wa Afrika Mashariki.

Hatua hii inafuatia kusainiana makubaliano ya awali baina ya Taasisi hizi mbili (Shirika la Posta Tanzania na Posta ya Oman) yaliyolenga kukuza biashara za posta kupitia ushirikiano wao. Makubaliano hayo yalitiliwa saini na Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Mbodo na Postamasta Mkuu wa Posta Oman Bw. Nasser Al Sharji, jijini Dar es Salaam yaliyofanywa Mei, 2022 na kushuhudiwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Moses Nnauye ambaye ndiye msimamizi wa Wizara yenye dhamana na Posta.

Hivyo, hatua hii ya pili makubaliano yanalenga kukuza Biashara Mtandao nchini na kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara mtandao kwa ukanda wa Afrika Mashariki.

Kupitia makubaliano hayo , upembuzi yakinifu sasa utafanywa ili kutoa mwelekeo wa kimkakati wa namna ya utekelezaji wa mradi huo na mikakati ya uwekezaji Tanzania kupitia Shirika la Posta huku ikihusisha kutathmini uwezekano wa kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara mtandao (E-commerce Hub) kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini.

Akielezea umuhimu wa hatua hii mpya katika ushirikiano wa kimkakati na Posta Oman, Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Mbodo amesema kuwa,

Shirika la Posta linaendelea kupanua wigo wake wa masoko kwa kuendeleza ushirikiano na mataifa mbalimbali duniani ikidhamiria kukuza biashara za mipakani na kuongeza wigo wa biashara za mtandao ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi wanapokuwa mahali popote duniani". Amesema Mbodo.




Kwa mara nyingine tena makubaliano hayo ya kibiashara yaliyofanyika Muscat, nchini Oman yameshuhudiwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Moses Nnauye huku makubaliano hayo yakiwekwa saini na Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Mbodo na Mkuu wa Posta ya Oman na Asyad Express, Nasser Al Sharji.

Aidha Mhe. Waziri Nape alikuwa nchini Oman kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kuhusu ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya Biashara Mtandao (E-Commerce Logistics) nchini kupitia Shirika la Posta Tanzania

Mhe. Nape aliambatana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Khadija Hamisi Rajabu, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (WHMTH) Mohammed Khamis Abdulla, Mkurugenzi wa Mawasiliano Wizara ya HMTH, Mhandisi Clarence Ichwekeleza, Mkurugenzi wa Uwekezaji kwa Umma, Lightness Mauki pamoja na Katibu wa Shirika la Posta Tanzania, Erick Maxmillian.

Chini ya makubaliano hayo Tanzania inatarajia kuwa na eneo maalum litakalotumika kwa shughuli za Biashara Mtandao sambamba na vitendea kazi vya kisasa ili kurahisisha huduma hiyo nchini. Vilevile Tanzania inatazamiwa kupata soko kubwa la biashara mtandao kutoka Oman, kupitia maduka makubwa duniani ambapo mizigo mingi hususani kwa ukanda wa Afrika mashariki itapitia nchini, hii itaongeza pato la Shirika la Taifa kwa ujumla.

Postamasta Mkuu Bw. Mbodo ameahidi kuendelea kushirikiana na kufanya kazi kwa karibu na Posta Oman ili kuwezesha huduma za Posta kuwafikia wateja wengi zaidi baina ya nchini hizi mbili na duniani kote sambamba na kuunganisha soko la Tanzania na Oman katika huduma za Mtandao.

# POSTA TANZANIA NA KONGO POSTA KUSHIRIKIANA BIASHARA MPAKANI

Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Mbodo ametoa wasilisho rasmi kuelezea fursa mbalimbali zinazopatikana nchini kupitia Shirika hilo, katika Kongamano la Fursa za Kibiashara na Uwekezaji katika sekta ya TEHAMA lililofanyika jijini Lubumbashi DRC.



Akieleza Fursa zinazopatikana wakati wa Kongamano hilo alitaja kuwa ni za Biashara Mipakani (Cross Boarder Trade) ikihusisha huduma za usafirishaji wa mizigo mikubwa na midogo pamoja na uwepo wa huduma ya Duka la kubadilisha Fedha (Bureau De Change) katika mpaka wa Tanzania na Congo.

Vilevile Postamasta Mkuu ameeleza fursa ya Duka Mtandao la Posta (E - Shop) linalowanufaisha wafanyabishara wakubwa na wadogo pamoja na wananchi kwa ujumla, kwani Duka hilo linawawezesha kuuza, kutangaza na kununua bidhaa mbalimbali mtandaoni na kufikishiwa mpaka mahali walipo.



Duka hilo lililounganishwa kwenye nchi 192 zilizopo chini ya Umoja wa Posta Duniani (UPU) lina lugha za kigeni zaidi ya 20 lengo ikiwa kurahisisha mawasiliano baina ya mteja na mfanyabiashara

Aidha, Kongamano hilo la siku mbili lililokuwa na zaidi ya washiriki 300 lilianza tarehe 18 Oktoba, 2022 na kuhudhuriwa na Taasisi mbalimbali za Tanzania linatarajiwa kuhitimishwa tarehe 19 Oktoba, 2022 huku likiwa na kauli mbiu ya "Kukuza Fursa za Mashirikiano, Biashara na Uwekezaji katika sekta ya TEHAMA" .





# UJUMBE WA TANZANIA WATEMBELEA POSTA USWISS

Ujumbe wa Tanzania ukiongozwa na Bi. Caroline Kanuti, Mkurugenzi Msaidizi, Huduma za Posta kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari umepata fursa ya kutembelea Posta ya mfano (Post of the Future), tarehe 27 Oktoba, 2022, nchini Uswiss.

Lengo la ziara hiyo ni kujionea mabadiliko na utendaji kazi wa Posta hiyo sambamba na kujifunza uendeshaji wa Posta za kisasa na kuutumia ujuzi huo katika kuimarisha na kuboresha Posta ya Tanzania katika kuwahudumia wananchi.

Aidha, Bi. Kanuti aliambatana na viongozi kutoka Shirika la Posta Tanzania akiwemo Meneja Mkuu Rasilimaliza za Shirika hilo Bw. Aron Oyye, Meneja Mkuu Uendeshaji Biashara Bw. Constantine Kasese, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Mambo Posta Kimataifa Bw. Elia Madulesi pamoja na wataalamu wa Uchumi wa Shirika hilo Bw. Tumaini Nguto na Suleiman Mwarabu

Wawakilishi wa Shirika la Posta Tanzania walikuwa nchini Uswiss kushiriki vikao vya mwaka vya Umoja wa Posta Duniani (UPU) vilivyoanza tarehe 17 Oktoba, 2022, nchini humo.

Tanzania ni mjumbe wa Mabaraza mawili ya maamuzi yanayoongoza Umoja huo yaani Baraza la Utawala lenye wajumbe 41 na lile la Uendeshaji lenye wajumbe 48, kupitia nafasi ambazo Tanzania ilizipata kwenye Mkutano Mkuu wa UPU Uliofanyika mwaka 2021 jijini Abidjan,Ivory Coast.





# TANZANIA NA OMAN KUSHIRIKIANA KATIKA SEKTA YA MAWASILIANO, HABARI NA TEKNOLOJIA

Tanzania na Oman zaweka mikakati ya ushirikiano katika sekta ya Mawasiliano, Habari na Teknolojia ambapo nchi hizi mbili zinaweza kutumia vyombo vyake vya habari kuhabarisha umma katika masuala mbalimbali ya kijamii, kutangaza tamaduni na kubadilishana ujuzi wa teknolojia.

Hayo yamebainishwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye wakati alipokutana na Waziri wa Habari wa Oman Mhe. Dkt. Abdullah bin Nasser bin Khalifa Al-Harassi tarehe 23 Novemba, 2022, nchini Oman.

Katika mazungumzo yao Waziri Mhe. Nape ameeleza kuwa, kutokana na mahusiano ya kihistoria ya muda mrefu kati ya Tanzania na Oman, nchi hizi zinapaswa kuhabarishwa ipasavyo juu ya undugu wa damu kati ya watu wa Oman na watanzania ili kuendelea kutunza uhusiano huo na kukubaliana kuwa Oman kupitia vyombo vyake vya habari itaitangaza Tanzania katika mataifa mengine ili kuvutia biashara, uwekezaji na utalii.

Aidha, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye alitembelea chumba maalum kinachotumika katika shughuli za uandaaji wa habari za magazeti, Radio na Televisheni kwa lengo la kufahamu uandaaji wa vipindi nchini humo.

Katika hatua nyingine, Waziri Nape alikutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Uchukuzi, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari wa Oman Mhe. Mhandisi Saeed Bin Hamoud bin Saeed Al Maawali huku Waziri wa Oman akiahidi kuendelea kuipa ushirikiano Tanzania katika Sekta ya Usafirishaji na Mawasiliano hususani katika masuala ya usalama mitandaoni (Cyber Security).

Vilevile Mhe. Nape alipata nafasi ya kutembelea maghala yanayomilikiwa na kampuni ya ASYAD EXPRESS na yanayotumika kutunzia bidhaa kwa ajili ya kusambaza na kuuza kwa wananchi kupitia biashara mtandao nchini Oman.

Sambamba na hilo, Mawaziri hao wawili wa Serikali ya Oman wameahidi kuendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kuboresha Habari; Mawasiliano na Teknolojia ya Usafirishaji kwa manufaa ya nchi hizi mbili.

# TANZANIA KUPITIA SHIRIKA LA POSTA INATARAJIA KUSAINI MAKUBALIANO YA KIBIASHARA SERIKALI YA DEKMOKRASIA YA CONGO

Tanzania kupitia Shirika lake la Posta inatarajia kusaini makubaliano ya kinoashara yanayolenga kuboresha bishara za mpakani (Cross boarder business) kupitia ziwa Tanganyika kutokea Kigoma kwenda DRC kupitia Kalemie jijini humo.

Hayo yameelezwa na Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Mbodo wakati aliposhiriki Kongamano la Fursa za Kibiashara na Uwekezaji katika Sekta ya TEHAMA lililofanyika tarehe 18 Oktoba, 2022, jijini Lubumbashi.

Wageni Rasmi katika Kongamano hilo walikuwa ni Mhe. Nape Nnauye, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyeongozana na Katibu Mkuu Wizara hiyo Dkt. Jim Yonazi na Mhe. Augustin Kibassa Maliba, Waziri wa Posta, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Akiwa katika Kongamano hilo, Postamasta mkuu ameeleza namna ambavyo Shirika la Posta nchini imejipanga kimkakati kushirikiana na Serikali ya DRC katika kuwahudumia wananchi wa Congo hususani kupitia Duka lake la Mtandao (E - Shop) linalowawezesha wananchi kuuza, kutangaza na kununua biidhaa mtandaoni mahali popote walipo.

Katika hatua nyingine Mbodo ameongeza kuwa, kutokana na fursa mbalimbali zilizopo Tanzania hasa kupitia Shirika la Posta nchini, Shirika la Posta linatarajia kusaini makubaliano ya mashirikiano katika maeneo mbalimbali ya kibiashara ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za Posta katika nchi zote mbili

Kongamano hilo lenye zaidi ya washiriki 300 lilihudhuriwa na Taasisi mbalimbali za Tanzania ikiwemo TAnTRADE, TTCL, Mamlaka ya Serikali Mtandao Tanzania, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Wizara ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Afrika Mashariki na TPSF.








Posta
Let's Go!

Tanzania Posts Corporation
Head Office: Posta House 12th Floor, 7 Ghana Street
P.O.Box 9551, 11300 Dar es Salaam, Tanzania
Fax: (022) 2113081 | Phone: 2113394/ 2111715/ 2118280
Mobile: +255 738 070 702 | Email: pmg@posta.co.tz
Web: www.posta.co.tz

@posta_tz